

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

S.L.P 30112,KIBAHA
SIMU Na: 023 - 2402886
FAX No: 023 - 2402007



OFISI YA MKURUGENZI
MJI WA KIBAHA

Kumb.Na. KTC/LD/PT/19546/9

26/03/2023

Kamishna wa Ardhi Msaidizi
Mkoa wa Pwani
S.L.P 9230,
DAR ES SALAAM.

**YAH: HISTORIA YA VIWANJA NAMBA 250 KITALU 'A' ENEO LA
MISUGUSUGU BAMBA- KIBAHA MJINI.**

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu.

Kihistoria eneo tajwa hapo juu lilikuwa likimilikiwa kimila na kampuni ya YMDY CO. LTD ya S.L.P 2040 DAR ES SALAAM kama ilivyothibitishwa na serikali ya mtaa wa MISUGUSUGU (muhtasari wa kikao umeambatanishwa). Awali eneo hili lilikuwa linamilikiwa na ndugu STEPHEN AUGUST ambaye baadae aliuza eneo hilo kwa ndugu YAN YANLI S.L.P 2040 DAR ES SALAAM ambaye pia ni mkurugenzi wa kampuni ya YMDY CO. LTD kwa gharama ya USD. Mia moja Hamsini na nane elfu mia nne (158,400.00) tu (mkataba wa mauzo umeambatanishwa) na kwamba taratibu zote za kuhamisha miliki hiyo ya kimila zilifuatwa.

Kampuni ya YMDY CO. LTD ya S.L.P 2040 DAR ES SALAAM ilitayarisha mchoro wa mipangomiji namba 31/76/092009C kwa matumizi ya VIWANDA VYA HUDUMA yaani SERVICE TRADE INDUSTRY na upimaji ulifanyika na kukamilika kwa kupewa namba ya ramani E'354/732 na kusajiliwa kwa namba 191935.

Kampuni ya YMDY CO. LTD ya S.L.P 2040 DAR ES SALAAM iliwasilisha kivuli cha cheti cha usajili wa kampuni pamoja na memorandum ya kampuni na baada ya kupitia kumbukumbu hizo ilibainika kuwa wakurugenzi wa kampuni sio raia wa Tanzania hivyo walitakiwa kuwa na kibali (Certificate of Incentive) chini ya kifungu namba 17 cha Sheria ya Uwekezaji namba 26 ya mwaka 1997 na walitimiza sharti hilo kwa kupewa certificate no. 022441136.

Kwa kuwa wamiliki wa kampuni husika ni rala wa kigeni, baada ya kukamilisha taratibu za makabidhiano na mmiliki wa asili nimeatayarishia Land Form no. 1 kwa ajili ya kutenga ardhi husika kuwa ardhi ya uwekezaji chini ya kituo cha uwekezaji kama sheria inavyoelekeza.

Baada ya taratibu husika za kuitangaza ardhi hiyo kukamilika, kiwanja hiki kimilikishwe kwa Tanzania Investment Centre ambao watatoa Derivative Right kwa YMDY CO. LTD kama sheria inavyoelekeza.

Nakutakia kazi njema.

Kennedy Mpanduji
Kny: MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA